



**Atakayesema: -Yaani: anapotoka nyumbani kwake-:
Bismillaahi tawakkaltu a'la Ilaahi -kwa jina la
Mwenyezi Mungu nimemtegemea Mwenyezi Mungu,
Laa haulaa walaa quwwata illaa billaa- hakuna ujanja
wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu,
huambiwa: Umeongozwa na umetoshelezwa na
umekingwa, na shetani hujitenga mbali naye**

Kutoka kwa Anas bin Maliki -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Hadithi Marfu'u:
"Atakayesema: -Yaani: anapotoka nyumbani kwake-: Bismillaahi tawakkaltu a'la Ilaahi -
kwa jina la Mwenyezi Mungu nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Laa haulaa walaa
quwwata illaa billaa- hakuna ujanja wala nguvu isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu,
huambiwa: Umeongozwa na umetoshelezwa na umekingwa, na shetani hujitenga mbali
naye". Ameongeza Abuudaudi: "Basi husema: -yaani shetani-: kuwaambia mashetani
wengine: utaweza vipi kwa mtu aliyeongozwa na akatoshelezwa na akakingwa?".

[Sahih] [Imepokelewa na Imamu Tirmidhiy - Imepokelewa na Abuu Daud]

Ameeleza Nabii -Rehema na Amani ziwe juu yake- kuwa mtu atakapotoka nyumbani kwake
na akasema: Bismillaahi -kwa jina la Mwenyezi Mungu-, Tawakkalu a'lallaahi -Nimemtegemea
Mwenyezi Mungu-, Laa haulaa walaa quwwata illaa billaahi- hakuna ujanja wala nguvu
isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, Malaika humuita Ewe mja wa Mwenyezi Mungu
umeongozwa katika njia ya haki, na umetoshelezwa mahitajio yako, na umehifadhiwa dhidi
ya maadui; basi shetani aliyewakilishwa kwake hujitenga mbali naye, na hapo husema
shetani mwingine kumwambia shetani huyu: utawezaje kumpoteza mtu tayari kaongozwa, na
katoshelezwa, na amekingwa na mashetani wote? kwasababu yeye amesema maneno haya
basi wewe hutomuweza.

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

